RAIA MWEMA
Jumatatu Oktoba 17, 2022

Ulaji vyakula vya asili ulivyohamasishwa Italia

Na Doreen Aloyce

SLOW Food International ni mtandao uliopo kwenye nchi zaidi ya 160 duniani unaojihusisha na wakulima wadogo katika kuhamasisha ulaji wa vyakula salama.

Mtandao huo ulianzishwa mwaka 1989 na Mwanaharakati Muitaliano anayejulikana kwa jina la Carlo Petrin kwa lengo la kukabiliana na changamoto zilizokuwa zimesababishwa na ulaji wa vyakula vya haraka (fast food).

Vyakula hivyo vilitengenezwa viwandani kwa kiasi kikubwa vimezalisha changamoto nyingi za kiafya kwa watu pamoja na kusababisha kusahaulika kwa vyakula vya asili.

Ili kukabiliana na hali hiyo mtandao huo ulianzishwa ili kuhakikisha watu wanapata chakula chenye radha nzuri inayoendana na utamaduni wao, kinachozalishwa kwa namna isiyoharibu mazingira na afya ya binadamu, lakini kinachomnufaisha pia mkulima ambaye ndio mzalishaji.

Aidha, mtandao huo wenye wanachama zaidi ya laki moja kutoka mataifa zaidi ya 160 duniani wanaofanya kazi pamoja lengo likiwa ni kulinda na kuhifadhi utamaduni.

Kila baada ya miaka miwili wanachama na wanaharakati wa mtandao huo kote duniani hukutana nchini Italia kubadilishana uzoefu na ujuzi juu ya uzalishaji, miradi na kufanya tathimini ya jinsi ambavyo shughuli za kilimo hai (organic) zimekuwa zikiendelea katika maeneo mbalimbali duniani.

Kupitia kongamano hilo maarufu kwa jina la Terra Madre watu mbalimbali hususani wakulima kutoka mataifa tofauti huambatana na bidhaa wanazolima kwa ajili ya maonesho na kujifunza aina ya vyakula ambapo pia watu hupata fursa ya kula vyakula kutoka mabara tofauti.

Katika kuendeleza mapambano hayo ya ulaji wa vyakula asili Slow Food International inaendelea kutoa mwito kwa wanajumuiya barani Afrika na duniani kwa ujumla kutumia mfumo wa 'Agro-Ecology' ambao ni uwezekano wa mabadiliko ya tabianchi duniani na uwezo wa kulisha Afrika ili kuboresha usalama wa chakula barani humo.

Vyakula vya asili

Aidha, mtandao huo unatoa mwito pia kwa wanajamii kuzalisha na kutumia vyakula visivyo na sumu katika miili yao vyakula vinavyoheshimu utamaduni kwa afya bora na endelevu ambao kwa kiasi kikubwa husaidia kuepuka magonjwa yanayosababishwa na ulaji mbaya.

Katika kongamano hilo ambalo limefanyika hivi karibuni Parco Dora mjini Turini, Italia umeenda sambamba na uchaguzi wa kiongozi mpya kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwa mtandao huo baada ya aliyekuwepo kumaliza muda wake kutokana na umri.

Akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kuhitimisha mkutano wa Terra Madre huko Parco Dora, Turin mwishoni mwa Septemba, mwaka huu, ambao ulikuwa wa wiki moja, Rais mpya wa Slow Food, Edward Mukiibi kutoka Uganda ameeleza kuwa, shirika hilo la mitandao linahamasisha vyakula bora safi vya haki pamoja na mfumo wa ikolojia ya kilimo, hatua inayolenga kutatua tatizo la usalama wa chakula linalodaiwa kusababishwa na mabadiliko ya tabianchi duniani.

"Kama unavyojua, Afrika haiwezi kutegemea mzunguko wa chakula duniani, hivyo matumizi ya mfumo wa ikolojia ya kilimo ni muhimu kwa usalama endelevu wa chakula," anaeleza.

Alifafanua zaidi kuwa, taasisi ya Slow Food inashirikiana na wakulima wadogo ili kuzuia kutoweka kwa tamaduni na mila za vyakula vya kienyeji, kukabiliana na ongezeko la maisha ya haraka na kupambana na kupungua kwa hamu ya watu katika chakula wanachokula, kinatoka wapi na jinsi vyakula vinavyoathiri ulimwengu unaotuzunguka.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, Slow Food inaamini kwamba chakula kinafungamana na nyanja nyingine nyingi za maisha, ikiwa ni pamoja na utamaduni, siasa, kilimo na mazingira.

"Kupitia uchaguzi wetu wa chakula tunaweza kushawishi kwa pamoja jinsi chakula kinavyolimwa, kuzalishwa, na kusambazwa," anaeleza.

Mukiibi anaeleza zaidi kuwa, matumizi sahihi ya ardhi katika uzalishaji wa chakula bora na safi ni muhimu kwa usalama endelevu wa chakula kutokana na mabadiliko ya tabianchi na kwamba Slow Food inashirikiana na wakulima wadogo kukabiliana na tatizo hilo.

Kwa upande wake, Valentina Meraviglia anasema kuwa mkutano wa Terra Madre umeonesha kwa mara nyingine kwamba pamoja na washiriki kutoka nchi 160 duniani kote, changamoto zilizopo wanapaswa kukabiliana nazo za kwa pamoja.

"Tukio hili limeimarisha uhusiano wetu na mshikamano, kuaminiana na kuimarisha azimio ambalo tunatekeleza lengo letu la pamoja la kupata kila mtu upatikanaji wa chakula bora, safi na cha haki," anaeleza na kuongeza kuwa:

"Kama vile Rais wetu Edward Mukiibi alivyosema kwamba suluhu za migogoro mingi tunayokabiliana nayo tayari zipo. Tumeziona, kuzisikia na kuzibadilisha kwa siku chache zilizopita na mamia ya wakulima, wapishi, wazalishaji wa chakula, wanaharakati na wataalamu waliokutana pamoja mjini Turini."

Naye Mratibu wa Shughuli za Slow Food Tanzania, Reguli Marandu akitoa maoni yake juu ya mkutano huo wa Terra Madre alimesema kuwa kongamano kama hilo ni muhimu sana kwa jamii ya sasa na vizazi vijavyo.

"Kama unavyoona wadau mbalimbali kuanzia wakulima wadogo kutoka Afrika, Amerika Kusini na kote ulimwenguni pamoja na mashirika muhimu katika sekta ya kilimo na chakula kama FAO na IFAD wote tumekutana hapa kujadili masuala mbalimbali ya usalama wa chakula, kilimo na mazingira na kutafuta suluhu ya changamoto katika mifumo yetu ya chakula," anasisitiza.

Marandu anasema kuwa mifumo ya uzalishaji chakula iliyojikita kwenye viwanda imekua ikiendelea kuathiri ardhi na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika mabadiliko ya tabianchi na zaidi kuganda miza wakulima wadogo.

Aliongeza kuwa kongamano hilo pia limetoa angalizo la upotevu wa vyakula vya asili ikiwa ni pamoja na wanyama wa asili huku akitolea mfano Tanzania kuna makabila zaidi ya 100 na kwamba kila kabila lina vyakula vyake vya asili, lakini vyakula vinavyoliwa kwa wingi kwasasa havizidi vyakula vitano.

"Tunapopoteza vyakula hivi sio chakula tuu kinapotea bali tunapoteza sehemu ya tamaduni zetu za asili, uhaba wa chakula ni changamoto kubwa sana Afrika na athari ya mabadiliko ya tabianchi kama ukame na mafuriko yanaongeza makali ya njaa," anasema.

wPia anasema kuwa ni muda sasa wadau wa kilimo na chakula kuanza kufikiria kuwekeza kwenye mifumo ya asili ya uzalishaji chakula, mifumo inayotumiwa na wakulima wadogo katika mashamba yao.

"Mifumo hii ya wakulima wadogo tayari inatumia dhana za kilimo ikolojia, kuna ujuzi fulani wakulima wadogo wamejifunza kwa uzoefu, hivyo ni wakati wa kujifunza kutoka kwao na kwa pamoja kuleta ustawi katika sekta ya kilimo na chakula," anasema.

Geofrey Ishengoma ni mkulima kijana kutoka Tanzania anasema kuwa kongamano limeenda vyema na ilikuwa ni nafasi adimu ya kukutana na washika dau kutoka maeneo mbalimbali duniani na kubadilishana uzoefu.